Utambuzi, Hisia na Mabadiliko ya Kisemantiki katika Leksia za Kiswahili

Tirus Mutwiri Gichuru, Kitula King'ei na *Ireri Mbaabu*
Chuo Kikuu Cha Kenyatta

Ikisiri

Makala haya yamejadili nafasi ya utambuzi na hisia katika mabadiliko kwenye kisemantiki ya leksia za Kiswahili. Makala yanaonyesha namna maarifa katika utambuzi hujenga msingi na kuongoza mbinu na taratibu mbalimbali za mabadiliko ya kisemantiki na hatimaye kuchangia katika mabadiliko ya maana. Mifano mahususi ya leksia kutoka Kiswahili cha kabla ya Karne ya Ishirini na cha Karne ya Ishirini na Moja imelinganishwa ili kudhihirisha mabadiliko husika. Asili ya data ni matini teule za kabla ya Karne ya Ishirini, matini za kilekskografia za Karne ya Ishirini na Moja na kutoka kwa wazungumzaji wa pwani ya Kenya wenye elimu-asilia. Nadharia ya Semantiki Tambuzi imezingatiwa. Imebainika kuwa tajriba na maarifa yaliyofichamwa kwenye utambuzi huwa nguzo muhimu katika kuleta mabadiliko ya maana za leksia. Makala haya pia yamedhihirisha mchango na ufaafu wa vigezo vya kiutambuzi vya nadharia ya Semantiki Tambuzi katika kuelezea mabadiliko ya lugha.

Maneno muhimu: Utambuzi, hisia, mabadiliko, leksia, Semantiki tambuzi

Utangulizi

Wanasaikolojia tambuzi hueleza kuwa mwanadamu hutumia mfumo wa kiutambuzi katika kuufasiri na kuudhibiti ulimwengu wake halisi na wa kidhahania (Lakoff na Mark, 1980; Croft na Cruse 2004). Kulingana nao utambuzi wa lugha ni sehemu ya mfumo wa utambuzi wa binadamu kwa ujumla na haishughulikiwi na sehemu ya kipekee au mahususi kando na tambuzi za masuala mengineyo kama ya kisaikolojia na hisia (Croft na Cruse, 2004; Vyvyan na Greeens, 2006; Lemmens, 2017). Kadhalika, nyenzo kuu za kujipa maarifa ni kupitia hisia tano za mwanadamu: kuona, kusikia, kugusa, kuonja na kunusa.Kwa mfano, mtoto anaanza kuelewa dhana ya 'ndani na nje' kupitia tajriba yake ya kuweka vitu 'ndani ya' mdomo wake. Maarifa haya huhifadhiwa katika 'ghala la maarifa' ambalo hujenga mfumo wa kiutambuzi. Maarifa ambayo tayari yamo kwenye tambuzi za wanajamii huwasaidia kukabili dhana mpya na mageuko

anuwai katika mfumo wa jamii. Mathalani, magari ya kivita ya kijeshi (vifaru) yalipoanza kutumika kwa mara ya kwanza katika vita vya kwanza vya dunia kati ya mwaka wa 1914 hadi 1918, Waswahili waliyaita magari haya ‘vifaru’ maadamu yalishabihiana kiumbo na mnyama aliyejulikana wazi katika mazingira yao. Ni wazi kuwa upanuzi wa upeo wa maana ulichochewa na kukitwa katika taswira ya mwono.

Fauka ya haya, dhana inapokosa matumizi, hutupiliwa mbali au kutumiwa kuwakilisha dhana nyingine tofauti. Kwa mfano, *gungu* ilikuwa sinia kubwa ya kizamani ya Waswahili iliyotengenezwa kwa shaba nyeupe yenye asili ya Kishirazi au Uajemi (Abdulaziz, 1979). Kabla ya karne ya 20, Waswahili waliipiga sinia hii kama ala katika nyimbo za harusi. Baadaye leksia *gungu* ilihamia kutoka *kifaa* hadi *ngoma yenyewe*. Maana mpya pekee ndiyo iliyo katika tambuzi za Waswahili wa kisasa. Katika TUKI (2013) ‘gungu’ inaelezwa kama ‘ngoma mojawapo ya kizamani ya watu wa mwambao wa Afrika Mashariki.’ Katika Unguja kulikuwa na *gungu la kufunda* iliyochezwa na mke na mume na *gungu la kukwaa* iliyochezwa na familia mbili ya mke na mume (Steere, 1870). Kuna mabadiliko ya aina mbili katika lugha: mabadiliko potevu na mabadiliko ingizi. Mabadiliko potevu ni mabadiliko ambayo kwayo neno hupotea kabisa au neno jipya huibuka na kutumika badala ya lile la zamani. Mabadiliko ingizi huwa mabadiliko ambapo msamiati huongezeka kwenye msamiati wa zamani. Msamiati mpya huingizwa katika lugha kwa njia ya kuunda maneno mapya au kutohoa kutoka lugha nyingine. Mabadiliko ya Kileksia katika Kiswahili yanahusisha mikondo mitatu mikuu kulingana na namna tatu za utokeaji:

(i) Uingizaji wa maneno mapya kwenye lugha kwa sababu hakuna maneno yanayowakilisha dhana husika. Kwa mfano, *kitanzambali* (kifaa kidogo cha kielektroni cha kuteua na kuthibiti mitambo kutoka mbali; rimoti).

(ii) Uingizaji wa maneno mapya ili yatumike sambamba na yale ambayo yapo. Kwa mfano, leksia *kompyuta, ngamizi* na *tarakilishi* hutumika sambamba.

(iii) Kupotea kwa maneno ya awali. Kuna baadhi ya leksia ambazo zilikuwa zikitumika zamani lakini kwa sasa leksia hizo hazitumiki tena huku nafasi yake ikichukuliwa na leksia mpya. Hii hapa ni mifano kutokana na Nabhany (2012):

(1)

Kikale	Kisasa
Gongwa	Ikulu
Ng’andu	Dhahabu
Ngeu	Damu
Utongolezi	Fitina
Tinene	Bara

Leksia nyingine katika (1) zilipotea katika matumizi na hupatikana tu katika tungo za kale. Msomaji yeyote wa matini za kabla ya Karne ya Ishirini anakumbana na leksia hizi. Wakati huohuo, anakumbana na leksia mpya zinazobuniwa kila kuchao kutokana na maendeleo na mabadiliko katika muundo wa jamii.

Suala la kubadilika kwa maana za leksia huchunguzwa katika tawi la isimu historia. Isimu historia hutalii mabadiliko mbalimbali ya lugha kadri miaka inavyopita. Mabadiliko ya lugha bila shaka huambatana na maendeleo na mabadiliko ya kijamii, kisiasa, kiuchumi kiteknolojia. Kiswahili sawa na lugha nyingine hakijasazwa na mabadiliko ya lugha katika viwango mbalimbali. Maumbo ya lugha yanapobadilika au kupotea hufanya maandishi yaliyopo kutoeleweka kwa urahisi hasa kwa wanaojifunza lugha kwa mara ya kwanza. Hali hii ndiyo inamkabili msomaji yeyote wa matini za kabla ya Karne ya Ishirini. Matini hizi zinaonekana kutumia maneno magumu na baadhi yake yamepotea katika tambuzi za watumiaji wa Kiswahili. Mathalani, Kiswahili kilichotumiwa katika *Kasida za Hamziyya, Al Inkishafi, Diwani ya Muyaka bin Haji* na *Utendi wa Fumo Liyongo* linatofautiana na Kiswahili kilichoko katika matini za karne ya Ishirini na moja. Kadhalika, kazi tangulizi za kilekskografia kama vile Steere (1870, 1919) na Krapf (1882) zinasheheni leksia ambazo katika matni za kisasa zina maana iliyobadilika. Kubadilika kwa maana leksia ni suala zito la kiisimu ambalo huathari muundo wa lugha.

Kuna wataalamu na wahakiki wengi walioshughulikia matini za kale za Kiswahili kama vile Hichens (1939), Harris (1962), Knappert (1979), Allen (1971), Abdulaziz (1979), Timammy na Swaleh (2013) miongoni mwa wengine. Hao walijikita kwenye fani mbalimbali za kifasihi zilizotumiwa katika tungo hizi. Kazi nyingi zilipendelea uchambuzi wa fani na maudhui bila kushughulikia kwa kina suala la mabadiliko ya maana katika mpito wa wakati. Ni hali hii ambayo imezua haja ya uchunguzi uliojikita katika mabadiliko ya maana za leksia mahususi za Kiswahili zilizopitia mabadiliko, kwa kufaidi vigezo mbalimbali vya kiutambuzi.

Data iliyochanganuliwa ilikusanywa kutoka kwa matini za kale za Kiswahili na nyingine kukusanywa kutoka kwa wahojiwa walio na ujuzi wa Kiswahili cha kale. Matini zifuatazo ziliteuliwa: Krapf (1882) *Dictionary of Suaheli Language;* Steere (1870). *A Handbook of the Swahili Language as Spoken at Zanzibar. Revised Edition* by *Madan (1919);* Burt (1910) *Swahili Grammar and Vocabulary;* Hichens (1939). *Al-Inkishafi; The Soul's awakening;* Allen (1971). *Tendi: Six examples of a Swahili Classical Verse form with Translations and Notes;* Abdulaziz (1979). *Muyaka 19th Century Swahili Popular Poetry;* Mutiso wa Kineene (2005). *Utenzi wa Hamziya;* Mulokozi (1999). *Tenzi Tatu za Kale;*Chiraghdin (1987). *Malenga wa Karne Moja na* Nabhany (2012) *Kandi ya Kiswahili.*

Kati ya leksia mia tano zilizokusanywa, sampuli ya leksia mia mbili iliainishwa na kupangwa katika makumbo ishirini na matatu kwa misingi ya uhusiano wa kimaana kama vile leksia za wanyama, za vifaa, za biashara na kadhalika. Leksia za Kiswahili cha kale kilichofifia na zingine ambazo zingali zinatumika katika Kiswahili cha kisasa kama vile *umeme*, *kanga* na *ndege*. Hata hivyo, katika makala haya tumeteua sampuli na kuchanganua mifano michache ambayo inaoana na malengo ya makala haya. Katika sehemu inayofuata tumeeleza kwa kifupi misingi ya nadharia iliyotuongoza katika utafiti huu.

Nadharia ya Semantiki Tambuzi

Nadharia ya Semantiki Tambuzi ni sehemu ya nadharia pana ya Isimu Tambuzi yenye asili yake katika Saikolojia Tambuzi (Vyvyan n.w. 2006). Mtazamo huu uliibuka katika miaka ya 1970 kwa sababu ya kutoridhika na mitazamo iliyotawala kipindi hicho na iliyotumia mfumo wa kanuni kufafanua lugha. Isimu Tambuzi ni mtazamo unaochunguza uhusiano kati ya maumbo ya lugha, akili na maumbo yanayopatikana katika mazingira na jamii (Vyvyan, keshatajwa; Lemmens 2017). Mtazamo huu huchunguza lugha kama chombo kinachorudufu fikira na kuakisi mfumo wa dhana na ruwaza ya fikira. Hutazama lugha kama mfanyiko wa kiakili sawa na hisia zingine za mwanadamu (Lee, 2001). Semantiki Tambuzi hushughulikia uhusiano kati ya tajriba, mfumo wa dhana na ruwaza za maana katika lugha. Kulingana na Lakoff (1987), Taylor (1999), Lee (ibid), Croft na Cruse (2004), Vyvyan et al (keshatajwa) na Lemmens (keshatajwa), mtazamo huu una misingi ifuatayo:

(i) Lugha kuwa sehemu ya utambuzi kwa ujumla

Kama tulivyotangulia kudokeza, utambuzi wa lugha ni sehemu ya mfumo wa utambuzi wa binadamu kwa ujumla (Croft na Cruse, 2004). Lugha haishughulikiwi na sehemu ya kipekee au mahususi kando na tambuzi za masuala mengineyo kama ya kisaikolojia na kihisia. Hakuna kifaa mahususi cha kiakili kinachoshughulikia lugha. Msimamo unaokinzana na madai ya wanasarufi-zalishi.

(ii) Kiini cha lugha huwa ni kuwasilisha maana

Semantiki Tambuzi hutambua kuwa kiini cha lugha ni kuwasilisha maana (Talmy, 2000). Maumbo yote ya lugha yamefumwa pamoja katika utambuzi kwa kusudi la kuwasilisha maana. Basi maana huwa katika majopo ya kiutambuzi. Maana haziwezi kuelezeka bila kurejelea utambuzi kwa ujumla. Kwa hivyo, maana si miliki tu ya leksia lakini mawanda yote ya utambuzi yana mchango katika kudhihirisha maana. Kimsingi, sarufi na leksia si hazina tofauti bali ni ncha mbili za upanga mmoja kama mchakato wa kudhihirisha maana. Vipengele vingine kama sifa za kiarudhi pamoja na sitiari pia hutoa mchango katika kufuma maana.

(iii) *Maana imejikita katika maumbile ya binadamu yakiwa msingi wa kufasiri dhana katika ulimwengu wake.*

Maana inaumbika katika tajriba za pamoja za watu zinazohusiana na maumbile ya binadamu. Maumbile na umbo lake binadamu humjengea binadamu misingi ya kutambua dhana mbalimbali katika mazingira yake, kile wanaisimu tambuzi huita picha au taswira (Vyvyan et al 2006; Lemmens 2017). Basi kifaa cha tingatinga cha kuchimbia na kupakia vitu watakiita *mkono wa tingatinga*. Wanadamu husimbua maana kutokana na namna wanavyofasiri dhana fulani. Kwa mfano, unapowauliza watu kadhaa walichokiona walipotembelea jijini Nairobi watatoa majibu anuwai kama vile waliona magari mengi, majumba marefu, bidhaa rahisi, barabara za kisasa, maduka mengi ya jumla, wachuuzi wengi kutegemea tajriba, usisitizo na madhumuni yao ya kutembelea jiji. Mhimili huu husaidia kueleza tofauti mbalimbali zinazochipuka kutoka na ufasiri wetu wa dhana moja. Pia unasaidia kueleza nafasi ya sitiari na lugha ya kimafumbo katika kuleta mabadiliko ya lugha.

(iv) *Maarifa ya kiutambuzi huwa katika kategoria zenye mizunguko na uzito (wa maana) ukififia kutoka kiinimaana.*

Maarifa aliyonayo mtu huwa yamehifadhiwa katika kategoria mbalimbali (Lee, 2001; Langacker, 2016). Vyvyan na Greens (2006) wanaelezea kuwa leksia ni chombo kinachotumiwa na wazungumzaji katika kufikia maarifa yaliyopo katika hifadhi ya maarifa katika utambuzi. Kwa mfano, neno 'paka' linapotamkwa humchochea mhusika kufikia maana ya msingi ya paka pamoja na masuala mengineyo yanayozunguka dhana hii kama vile familia mbalimbali za paka, sauti na chakula wakipendacho. Aidha neno 'mama' lina maana msingi yaani 'aliyezaa kiumbe fulani.' Hata hivyo, maana hii msingi imeambatanishwa na maana zingine za neno mama kama vile mama wa kambo, mama mlezi, mama mkwe na kadhalika. Maarifa haya, kwa ujumla hujenga mizunguko ya kategoria kuhusu maana ya neno 'mama'. Uzito wa maana hufifia ukiondoka nje ya kiinimaana au maana msingi (Lakoff, 1997; Croft na Cruse, 2004). Dhana hii ilisaidia kueleza namna maana msingi huweza kupishana nafasi na maana za ziada. Pia inatusaidia kuelezea kufifia kwa maana na nafasi ya metonimu katika mabadiliko ya maana leksia. Mizunguko ya maana inakuwa muhimu katika kuelezea uhusiano wa kipolisemia wa maana.

(v) *Lugha huhusisha ujenzi wa picha za mawazo na mipaka ya kidhana katika mawanda ya kiutambuzi.*

Utambuzi na matumizi ya lugha huhusu ujenzi wa mipaka ya kidhana (Lemmens, 2017). Binadamu ana uwezo wa kuhamisha dhana mbalimbali kidhahania kupitia sitiari, jazanda, metonimu na uhulutishaji (Croft, 1993). Kulingana na wanaisimu-tambuzi, sitiari ni mchakato wa kuhamisha dhana kutoka kwa uwanda moja na kuipachika kwa dhana tofauti ya nyanda zingine (Lakoff na Mark, 1980).

Kuhusu uhulutishaji, mawanda mawili yanatoa dhana inayounda dhana tofauti katika uwanda mwingine. Mhimili huu unasaidia kuelezea mabadiliko ya maana leksia yanayoletwa na matumizi ya jazanda au sitiari, lugha ya kimafumbo, tasfida, metonimu na uhulutishaji. Huu ndio msingi wa mabadiliko ya maana kileksia.

(vi) Maana hujikita katika kaida na tajriba za pamoja; ina sifa za kitamaduni
Isimu tambuzi hutambua maana iliyojikita kwenye tajriba (Vyvyan na Greens, 2004). Maana ya maumbo ya lugha huibuka katika jamii na utamaduni wa watumiaji wa lugha (Päivi na Maria, 2016). Kwa hivyo, wanaisimu tambuzi huzingatia mtazamo-tumizi katika uchanganuzi wa lugha. Mtazamo huu hushikilia kuwa kuna kufanana kwa kiasi kwa namna ambavyo watu hutumia lugha. Wao huiga na kuathiriana kilugha. Mhimili huu unasaidia kufafanua mabadiliko yanayoletwa na lugha ya mafumbo na tasfida, athari za lugha za kigeni na suala la kuiga mitindo mbalimbali ya lugha ambayo pia huleta mabadiliko ya maana kileksia.

(vii) Maana huwa na muundo wa kiensaiklopidia
Maana hujumuisha maana msingi pamoja na fahiwa zake zote (Geeraerts Mha., 2006; Lemmens, 2017). Japo kuna maana moja kuu ya kileksia, anayejua maana ya leksia fulani pia hujua maelezo mengineyo mengi yanayoambatanishwa na leksia hiyo. Vilevile, hakuna mipaka mahususi na bayana kati ya maana ya leksia na utambuzi unaotokana na maana hiyo. Kwa hivyo maana ya leksia fulani ni maana kuu pamoja na maelezo ya matumizi yake katika miktadha anuwai ya jamii. Hii ndiyo maana ya kiensaiklopidia. Maana ya leksia fulani haiwezi kueleweka kikamilifu bila kuhusisha maarifa ya kiensaiklopidia ya leksia hiyo. Kwa hivyo, aliye na umilisi wa dhana 'simba' pia hutambua sifa zake kama vile ujasiri wake, angurumavyo, sura yake, chakula akipendacho na familia yake. Lee (2001) anaeleza kuwa kubadilika kwa upeo wa maarifa, usisitizo, kuipa dhana mahsusi kipaumbele na sitiari huchangia pakubwa kuleta mabadiliko ya lugha. Katika kauli: *Yeye (A) ni simba (B),* sifa ya *ujasiri* ndiyo imepewa kipaumbele licha ya mnyama husika kuwa na sifa nyinginezo. Pia mmilisi wa lugha atatambua kuwa anayerejelewa (A) ni binadamu na si mnyama.Mhimili huu unasaidia kueleza mahusiano ya maana asili na maana mpya zinazoambatanishwa na dhana fulani; kihalisia au kitamathali.

Uchanganuzi na Matokeo

Uchanganuzi wa data ulihusisha kutambua leksia zilizobadilika kimaana na kubainisha mbinu za mabadiliko ya kisemantiki zilizohusika. Uchanganuzi ulibainisha bayana kuwa mabadiliko ya maana za leksia si suala la kiholela bali yaliambatana na mifanyiko mbalimbali ya kiutambuzi. Wanasemantiki tambuzi hueleza kuwa binadamu ana uwezo wa kuhamisha dhana toka kitu au dhana moja

hadi kitu au dhana nyingine katika mawanda ya kiutambuzi. Maarifa ambayo tayari yako katika tambuzi zao hujenga msingi wa kuelezea dhana mpya kwa kutumia uwezo wao wa kuunda picha au taswira; kile Lakoff (1987) anakiita sitiari. Kinachohamishwa huwa tabia, taswira ya umbo au kazi ya kitu kwa kuihusisha na tabia au umbo au kazi ya kitu kingine. Kipacha (2005) alisema kuwa sitiari ina muundo ufuatao: mada (kizungumzwa), taswira (kifananishi) na ufanano (kiungo). Zingatia jedwali lifuatalo:

Jedwali 1: Muundo wa Sitiari: Mada, Taswira na Ufanano

Mada (Kizungumziwa)	**Taswira (Kifananishi)**	**Ufanano (Kiungo)**
Stima	**Umeme**	Mwangaza
Kiingilio	**Mdomo**	Uwazi, upenyo
Uongozi	**Simba**	Ujasiri
Mke	**Jiko**	Upishi
Riziki	**Unga**	Hulisha mtu
Bidii	**Jasho**	Huzalisha riziki

Katika mifano hii, lugha ya kitaswira ilihusika kuleta mabadiliko yanayotokana na ufanano wa aina fulani. Ni wazi kuwa maarifa aliyonayo mtu, humjengea msingi wa kufasiri ulimwengu wake halisi au wa kidhahania. Uchanganuzi ulibainisha kuwa maumbile ya mwanadamu humjengea msingi wa kuufasiri ulimwengu wake. Zingatia mifano ifuatayo:

(1)

Sehemu ya mwili	*Maana ya Kimsingi*	*Maana mpya*
Kichwa	Kiungo juu ya shingo	Kiongozi, kinara
Mdomo	Uwazi wa kulia/kinywa	Uwazi katika kifaa ~ wa chupa
Jicho	Kiungo kionacho/maninga	Pambo kwenye omo/gubeti ya jahazi
Moyo	Mtima	Kiini cha mti
Ulimi	kiungo ndani ya kinywa	Lugha

Maana-msingi na maana ya awali ya *tumbo* ni 'sehemu inayofanana na **mfuko** iliyo **ndani** ya viumbe ambayo inapokea na kukisaga chakula'. Baadaye leksia hii ilibadilika ikapata maana ya jumla na kuwa: 'sehemu (yote) ya kiwiliwili iliyo kati ya kifua na kinena.*'* Kwa ufupi, leksia msingi imepanuka na kuhusisha dhana za kandokando kama inavyodhihirishwa katika kielelezo kifuatacho:

Kielelezo 1: Mageuko ya 'tumbo' kutoka Kiini- Maana



Maana inapotokea kuwa ya jumla, basi mbinu ya mabadiliko ya kisemantiki iliyohusika ni *semantiki panuzi* na *sitiari*. Uchanganuzi pia ulibainisha kuwa hisia tano za mwanadamu za kuona, kusikia, kuonya, kugusa na kunusa zina nafasi muhimu katika mabadiliko ya maana za leksia za Kiswahili. Hisia hizi husaidia kujenga taswira katika hali halisi au kidhahania. Hii hapa ni mifano inayohusiana na taswira ya mwono:

(i) Mabadiliko kupitia Taswira ya Mwono

Binadamu anapoona kitu kinachoshabihiana na kingine anachokijua, huwa mwepesi wa kutambua uhusiano kati ya dhana zote mbili kianalojia kupitia picha au taswira. Aidha, binadamu ana uwezo wa kiutambuzi wa kuhamisha dhana kutoka wanda moja la maarifa hadi jingine (Lakoff na Mark, 1980). Hali hii husababisha upanuzi wa upeo wa maana ya leksia zinazohusika. Basi maana mpya ya leksia inahusiana na ya awali kihistoria kupitia *uhusiano wa kisitiari*. Ikumbukwe kuwa dhana zinazohusishwa kimwono zinaweza kuwa za kiumbo, maumbile, matumizi, hulka, kiwango, mahali au mwendo mradi zinaonekana. Hii hapa ni mifano ya leksia zilizobadilika kupitia taswira ya mwono licha ya kuwa katika mawanda tofauti. Tazama picha ifuatayo kwa makini:

Picha 1:Pembe za Mnyama na Maumbo yake Nyambulishi

Mnyama Pembe tatu Pembe nne pembe tano



Dhana asilia iliyokuwa katika tambuzi za Waswahili ni pembe za wanyama ambazo huwa na ncha kali. Taswira ya mwono ndiyo imezingatiwa kuyapa majina maumbo yaliyoambatanisha, hali iliyopanua maana ya leksia pembe. Tazama picha nyingine:

Picha 2: Kanga (Ndege) na Kanga (Leso)



Maana asilia ya *kanga* ni 'aina ya nyuni wa jamii ya kuku anayeishi porini, mwenye rangi ya kijivu iliyokoza na madoadoa.' Leksia hii pia hupatikana katika lugha zingine za Kibantu; *nkanga* (Kinzuani, Kipokomo, Kimeru, Kikuyu); *nkaanga* (Ki-Mwiini); *k*^{h}*anga* (Kiduruma, Kiamu, Kimvita); *nkanga-dungwe* (Ngazija); *anga* (Kimwani). Leksia hii ingali inatumika katika Kiswahili Sanifu kwa maana hiihii (TUKI 2013). Leksia 'kanga' ilipanuka kimaana kutajia *vazi maalum* yaani 'aina ya nguo nyepesi yenye nakshi na maandishi inayovaliwa na wanawake, leso' (Abdulaziz, 1979; National Museums of Kenya, 2005). Pia tazama picha ifuatayo:

Picha 3: Vifaru

Maana ya leksia *kifaru* ilibadilika katika karne ya ishirini kuwakilisha gari la chuma la kivita lenye mzinga katika sehemu yake ya mbele. Gari lenyewe hutumiwa na wanajeshi kutupia makombora. Vifaru vilitumiwa kwa mara ya kwanza na Ufalme wa Muungano wakati wa vita vya kwanza vya dunia (1914-1918) dhidi ya Wajerumani. Huenda mabadiliko haya yalitokea wakati huo.Taswira ya kuona iliyojengeka Waswahili walipoona kifaru (gari) kwa mara, ilisimbua maarifa ambayo tayari walikuwa nayo katika tambuzi zao kuhusu kifaru (mnyama). Tazama picha nyingine:

Picha 4: Aina za Ndege

Leksia *ndege* ilitumika katika lahaja ya Kiunguja (Burt, 1910). Mabadiliko yanatokana na kuingia kwa eropleni katika mazingira ya Afrika Mashariki baada ya kufika kwa Wakoloni. Mabadiliko haya yalitokea katika kipindi cha nusu ya kwanza, ya karne ya Ishirini. Kuwepo kwa 'mbawa' katika chombo hiki na uwezo wa kupaa angani kulichochea Waswahili kuhamisha maana kutoka wanda moja kwa lingine la kiutambuzi. Uhusiano unaodhihirika katika picha 1-4 ni wa kihistoria yaani dhana B ina asili katika A. Mkondo huu ndio uliozingatiwa katika mabadiliko ya kisemantiki ya leksia zifuatazo:

(2)

<u>Leksia</u>	**A**	**B**
-lango	Kiingilio cha nyumba au mji	> Mahali pa kufungia bao katika soka
Ulingo	Jukwaa la kulindia shamba	> Jukwaa la michezo ~ *wa masumbwi*
Umeme	Mwanga uandamwao na radi	> Nguvu za stima au betri
Kupe	Mdudu afyonzaye damu	> Mtu mtegemezi
Tamba	Tembea, safari	> Tembea kwa majisifu, simulia
(U)tatu	Mbili kuongeza moja	> Shairi la mishororo mitatu katika beti

Maana za leksia katika B zina historia yake katika A. Basi kuwepo kwa umbo A ndio msingi wa kuwepo kwa umbo B.

(ii) Mabadiliko kupitia Taswira ya Mguso

Mabadiliko mengine hutegemea utambuzi kupitia hisia za mguso. Mathalani, *msasa* ni aina ya mti wenye majani yenye mguso wa kukwaruza. Awali majani haya yalitumiwa na seremala kulainishia vitu vya mbao (Krapf, 1882). Katika Kiswahili cha kisasa, msasa ni karatasi maalum iliyotiwa chembechembe za mchanga inayotumiwa na seremala ya mguso ya ukwaruzo' ndiyo imetumika kufanikisha badiliko hili. 'Kupiga mambo msasa'ni tamathali yenye maana ya kulainisha au kurekebisha mambo. Kadhalika, kitenzi 'saga' kilikuwa na maana ya kupondaponda kitu hadi kiwe mfano wa ungaunga; sababisha kitu kiishe polepole kwa kukisugua na kingine (Krapf, 1882). Awali, Waswahili walisaga nafaka kwa *mawe ya kusagia*. Jiwe kubwa la chini liliitwa *mama* na dogo la juu likiitwa *mwana* (Johnson, 1939). Katika mwisho wa karne ya ishirini, kitenzi –saga kilianza kutumika kama tasfida ya 'kitendo cha kufanya ngono kati ya wanawake wawili kwa kugusanisha uke wao ili kujifurahisha' (Longhorn, 2011). Msagaji basi ni mwanamke anayejamiiana na mwanamke mwingine bila shaka kwa kugusisha sehemu za uke. Basi kuna mshabaha wa jinsi tendo la awali na tendo jipya hufanyika kupitia taswira ya mguso. Mbinu ya mabadiliko ya kisemantiki ni *upanuzi wa maana kisitiari, udhalilikaji na tasfida.*

Fauka ya hayo, kitenzi 'saga' kilikuwa na maana msingi ya *kupondaponda kitu hadi kiwe mfano wa ungaunga, sababisha kitu kiishe polepole kwa kukisugua na kingine* (Krapf, 1882). Awali Waswahili walisaga nafaka kwa mawe ya kusagia. Jiwe kubwa la chini liliitwa mama na dogo la juu likiitwa mwana (Johnson, 1939). Katika mwisho wa Karne ya Ishirini, kitenzi *saga* kilianza kutumika kama tasfida ya 'kitendo cha kufanya ngono kati ya wanawake wawili kwa kugusanisha uke wao ili kujifurahisha' (Longhorn, 2011). Basi msagaji ni mwanamke anayejamiiana na mwanamke mwingine. Kuna mshabaha wa jinsi tendo la awali na tendo jipya hufanyika kupitia taswira ya mguso. Mbinu za mabadiliko ya kisemantiki zilizokupitia mbinu ya upanuzi wa maana kisitiari, udhalilikaji na tasfida.

Maana ya awali ya 'kereketa' ni *patwa na mwasho kooni au kinywani kama ifanyavyo tumbako kwa pua au mdomo, au mchanga unapoingia kwa macho*

(Steere, 1870; Krapf, 1882; Burt, 1910). Hivi leo, leksia hii imetwikwa maana za ziada yaani, *jambo la kuudhi, tetea jambo fulani kwa dhati baada ya kuchukua msimamo mkali.* Mabadiliko ya leksia yametiwa kasi na wanaharakati wa mashirika yasiyo ya kiserikali ya kutetea haki za wanajamii ambapo walipewa lakabu 'wakereketwa' na watetezi wa haki za binadamu. Uteuzi wa leksia hii huonesha misimamo sugu isiyotetereka. Leksia *kereketa* isikanganywe na *keketa,* iliyoingia hivi majuzi katika Kiswahili,yenye maana*; tafuna kitu, kuumwa na tumbo sana, kata kitu kigumu kwa kutumia kisu butu, tahiri mwanawake* (BAKITA, 2015). Maana inayoonekana kupewa kipaumbele katika kisasa hasa kwa wanaharakati wanaotetea haki za wanawake ni *tendo la kutahiri* m*wanawake*. Mabadiliko ya kisemantiki yanayohusika ni ya upigaji *chuku* na *sitiari*.

Maana ya awali ya 'usugu', kutokana na kitenzi 'kusugua' ni ugumu wa ngozi utokanao na msuguano baina ya viungo. Pia, usugu hutokana na vidole kusuguana na viatu. Krapf (1882) anasema 'sugu' ni mahali pagumu. Katika kisasa leksia hii imepata maana za ziada: *tabia ya ukaidi, -sioweza kuondolewa kwa urahisi. -enye kustahimili, -kutosikia adhabu au dawa, isiyobadilika kwa urahisi*. Msimamo ~, imani ~ ugonjwa ~. Hapa, maana ya leksia *imekuwaya jumla.* Pia inatumiwa *kisitiari*.

(iii) Mabadiliko kupitia Taswira ya Mwonjo

Maana awali ya *mtindi* imekuwa 'maziwa yaliyoganda na kupata ukali' (Krapf, 1882). Pia ni maziwa yanayobaki baada ya kutolewa siagi. Katika kisasa leksia husika imebadilika kimaana na kupata maana ya ziada yaani *pombe.* Nahau *piga mtindi (kunywa pombe)*. Hapa leksia imehama kisitiari ambapo 'maziwa' huwakilisha 'pombe.' Mabadiliko hayo yalinuia kutumia lugha ya kitasfida kuhepa hisia zisizofaa zinazohusishwa na pombe hasa ile haramu. Mbinu ya mabadiliko ya kisemantiki ni *sitiari* na *tasfida*. Aidha, maana ya awali ya *uroda* ilikuwa *–enye raha, inayopendeza* (Massamba, 2004). Maana ya kisasa ya 'uroda' ni *tendo la kujamiiana* (TUKI, 2013). Mbinu ya mabadiliko ya kisemantiki ni *tasfida* na *udhalilikaji wa maana.* Pia, keki ni mkate wenye sukari nyingi hutumiwa katika kisasa kama sitiari ya 'rasilimali' mathalani katika *kauli ~ ya taifa*.

(iv) Mabadiliko kupitia Taswira ya Kusikia

Maana ya msingi ya kitenzi-*endesha* ni kitendo cha kuongoza chombo cha usafiri kama gari, baiskeli na kadhalika kuelekea mahali fulani. Bila shaka mwendo wa vyombo vya usafiri huandamana na kelele fulani. Katika lugha ya hadhi kitenzi hiki hutumiwa kitasfida kuwakilisha dhana yenye aibu ya 'kuhara.' Inaonekana tendo lenyewe limepigwa *chuku*. Muharo mwepesi hujulikana kama 'parata' (Nabhany, 2012). Mabadiliko haya yalihusu *upanuzi wa maana* kupitia *chuku,tasfida* na *udhalilikaji wa maana*. Kadhalika, maana ya awali ya 'foka' ni

kitendo chamaji au pombe kuchemka na kutoa mapovu hadi kumwagika, maji kutoka kwa nguvu kupitia kwa tundu, bubujika. Hivi leo, leksia hii ina maana ya ziada yaani, *sema kwa harakaharaka na kwa hasira, sema kwa ukali*. Katika mabadiliko haya, tendo la kuteta linamithilishwa na tendo la kufoka kwa maji au pombe. Mbinu ya mabadiliko ya kisemantiki ni *upanuzi wa maana kisitiari* na *udhalilikaji.*

(v) Mabadiliko kupitia Taswira ya Mnuso

Kama tulivyotangulia kusema, maana za leksia huwa na muundo wa kiensaiklopidia. Basi leksia *choo* inapotajwa huchochea (katika akili ya msikilizaji) maswala mengiyo yanayoambatana na dhana husika, kwa mfano, harufu chukizi itokanayo na kinyesi, kilindi/shimo au kijumba kilicho pembeni chenye nzi wengi, maji ya kuoga na kadhalika, kulingana na tajriba ya mhusika. Waswahili huona aibu kutaja maneno *mavi* na badala yake kutumia lugha ya kimafumbo. Maana msingi ya choo ni 'chumba au mahala pa kujisaidia' lakini ilibadilika na kupanuka kiupeo kupitia mkondo ufuatao:

Mahali/chumba pa kujisaidia > mavi > mambo ya upuzi, ya kijinga

Katika badiliko la kwanza, leksia *choo* imetumika kitasfida na kimetonimu ambapo dhana pana (chumba) inawakilisha dhana finyu (mavi). Matumizi ya choo kuwakilisha 'mambo ya upuzi, ya kijinga au maovu' ni ya kisitiari ambapo dhana ya mnuko ndiyo imetumiwa katika kudhalilisha maswala yanayorejerewa. Kuna leksia zingine zinazohusiana na dhana ya 'choo' ambazo zimebadilika kwa sababu ya tasfida. Maana ya awali ya msala**ni** (**-ni -** kielezi cha mahali) ilikuwa ilikuwa *musalla*, lenye maana ya 'mahali pa kusalia' kisha ikasogea kwa 'mkeka *wa duara au zulia dogo la kuswalia*' na hatimaye ikaanza kutumiwa kama tasfida ya 'chooni' (Burt, 1910; Akidah, 2013). Katika Kiswahili cha karne ya 21, *msalani ni mahali pa usafi, chumba maalum ambapo watu huenda haja, chooni. Ameenda ~.* Leksia nyingine zinazoboresha dhana ya choo ni pamoja na *kwenda haja* na *kujisaidia.*

Uchanganuzi ulibainisha kuwa kuna leksia nyingine ambazo hubadilika kwa kuchochewa na masuala mengineyo yaliyo nje ya hisia tano za mwanadamu kwa mfano, *kipusa* (upembe wa kifaru) >*msichana mrembo*. Badiliko hili linatokana na 'thamani' iliyoambatanishwa kwa dhana hizi na si 'urembo' unaoonekana kwa macho halisi. Huu ni uwezo wa kiutambuzi.

Hitimisho

Makala haya yamebainisha wazi kuwa maarifa na tajriba zilizofichamwa kwenye utambuzi huwa nguzo muhimu katika kuleta mabadiliko ya maana za leksia. Imebainika wazi kuwa muundo wa maana na maumbile ya mwanadamu hasa hisia zake tano na ufasili wake wa ulimwengu wake husaidia mwanadamu kukabiliana na dhana mpya zinazoibuka katika mazingira halisi na ya kidhahania.

Imebainika kuwa maana imefumwa katika historia, falsafa na tajriba za pamoja za wanajamii; ina sifa za kitamaduni. Utambuzi huwa 'ghala' la maarifa aliyo nayo mtu (au jamii) ambayo kila kuchao huzidi kupanuka kiupeo, kufinyika na kugeuka kuambatana na maswala yanayomzunguka. Kadhalika, fasili tofauti za dhana moja, usisitizo na dhana kupewa kipaumbele ni masuala yachangiayo mabadiliko ya lugha. Mwisho, makala yameonyesha mchango na ufaafu wa vigezo vya kiutambuzi vya nadharia ya Semantiki Tambuzi katika kuelezea mabadiliko ya lugha. Yamkini maana huwa sehemu ya utambuzi kwa jumla sawa na maswala mengine kama hisia.

Marejeleo

Abdulaziz, M. H. (1979). *Muyaka 19th Century Swahili Popular Poetry.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Akidah, M. A. (2013). 'Phonological and Semantic Changes in Language Borrowing: The Case of Arabic words Borrowed Into Kiswahili' in *International Journal of Education and Research* Vol. 1, No. 4. University of Nairobi.

Allen, J.W. T. (1971). *Tendi: Six Examples of a Swahili Classical Verse Form with Translations and Notes.* Nairobi: Heinemann.

BAKITA (2015). *Kamusi Kuu ya Kiswahili.* Nairobi: Longhorn Publishers Limited.

Burt, F. (1910). *Swahili Grammar and Vocabulary.* London. Society For Promoting Christian Knowledge Northumberland Avenue, W.C.

Chiraghdin, S. (1987). *Malenga wa Karne Moja*. Nairobi: Longman Kenya limited.

Croft, W. and Cruse, A. (2004). *Cognitive Linguistics*: Cambridge: Cambridge University Press.

E.A.E.P. (2011). *Comprehensive Swahili – English Dictionary*. Nairobi: E.A.E.P. Limited.

Fromkin, Rodman na Hyams (2011). *An Introduction to Language and Linguistics*, 9th edition. USA: Wadsworth Cengage learning.

Geeraerts, D., ed. (2006). *Cognitive Linguistics: Basic Readings*. Berlin / New York: Mouton de Gruyter.

Harris, L. (1962). *Swahili Poetry*. Oxford. The Clarendon Press.

Hichens, W. (1939, 1972). *Al-Inkishafi: The Soul Awakening*. Nairobi: Oxford University Press.

Johnson, F. (1939). *A Standard Swahili-English Dictionary.* Oxford: Oxford University Press.

Kineene wa Mutiso (2005). *Utenzi wa Hamziya*. Dar es Salaam: TUKI

Kipacha, A. (2005). *Utangulizi wa Lugha na Isimu. OSW 101*. Dar es Salaam. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Knappert, J. (1979). *Four Centuries of Swahili Verse*. London: Heinemann.

Krapf, J. L. (1882). *Dictionary of Suaheli Language*. London: Trubner and Co. Ludgate Hill.

Langacker, R. W. (2016). *Entrenchment in Cognitive Grammar*. Washington: De Gruyter Inc.

Lakoff, G. & Mark, J. (1980). *Metaphor we Live by*. Chicago: Chicago University Press.

Lee, D. (2001). *Cognitive Linguistics; An Introduction*. Oxford: Oxford University Press.

Lemmens, M. (2017). 'Cognitive Semantics' in *Routledge Handbook of Semantics*. Editor Nick Riemer. London and New York: Routledge.

National Meuseums of Kenya (2005). Interactive Project: Swahili Attire Exhibition.

Massamba, D.P. (Mhariri) 2004. *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam: TUKI.

Mulokozi, M. M. (Mhariri) 1999. *Tenzi Tatu za Kale*. Dar es Salaam: TUKI.

Nabhany, S. A. (2012). *Kandi ya Kiswahili*. Aera Kiswahili Researched Products. Dar es Salaam.

Päivi J. and Maria K. eds (2016). *The Lexical Typology of Semantic Swifts*. Washington: De Gruyter inc.

Polome, E. (1967). *Swahili Language Handbook*. Washington: Centre for Applied Linguistics.

Steere, E. (1870). *A Handbook of the Swahili Language as Spoken at Zanzibar. Revised Edition* by *Madan (1919).* London: Society for Promotion of Christian Knowledge.

Talmy, L. (2000). *Towards Cognitive Semantics; Vol. 1: Concept structuring Systems.* Cambridge: MIT Press.

Timammy, R. na Swaleh, A. (2013). 'A Thematic Analysis of Utendi wa Kupona: A Swahili/Islamic perspective' in *Journal of Education and Practice.* Vol. 4. No 4.

TUKI (2004, 2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.

Vyvyan, E. and Greens, M. (2006). *Cognitive Linguistics. An Introduction*. Edinburgh: Edinburgh University Press.